KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 18, Issue 1
12th Safar 1433
6th Jan, 2012

KUHUKUMIANA KWA AMBAYO HAYAKUTEREMSHWA KUTOKA KWA ALLAAH [Imaam Ibn al-Qayyim]

UKAFIRI:
Amma kuhusu ukafiri, umegawanyika sehemu mbili.
Kufr Akbar (ukafiri Mkubwa), na Kufr Asghar (ukafiri mdogo)
Kufr Akbar – (Ukafiri) Huu unashurutisha kudumu motoni milele, na Kufr Asghar – Huu unashurutisha utimizaji wa makemeo (ya motoni) pasi na kuwemo humo milele. Kama ilivyo kwenye maneno yake Allaah (سبحانه وتعالى) nayo yalikuwa ni miongoni mwa yenye kusomwa kisha yakafutwa: **"Na wala musiwatukane baba zenu, kwani huo ni ukafiri utokao kwenu."** Na maneno yake Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Kuna mambo sampuli mbili katika Umma wangu, utawatia kwenye ukafiri; kutukana nasaba na kuomboleza kwa makelele (kumlilia maiti)."
Na maneno yake kwenye sunan: "Yoyote atakaemuingilia Mkewe kwenye tupu yake ya nyuma atakuwa ameyakufuru yote aliyoteremshiwa Muhammad (صلى الله عليه وسلم)" na katika hadeeth nyengine: "Yoyote atakaekwenda kwa mpiga ramli (mchawi) na akamuamini kwa ayasemayo atakuwa ameyakufuru yote aliyoyateremsha Allaah kwa Muhammad." Na maenno yake: "Musiwe ni makafiri baada ya kuondoka mimi, kwa kukatana shingo zenu wenyewe kwa wenyewe."
Na haya ndiyo maelezo ya Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) na kwa ujumla ya Maswahaba kuhusiana na maneno ya Allaah: **"Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Allaah, basi hao ndio makafiri."** (5:44). Ibn Abbaas akasema: "Huu si ukafiri wenye kumtoa mtu nje ya Dini. Bali pindi anapoufanya (ukafiri huo), basi inakuwa ni [kitendo cha] ukafiri, na wala yeye si kama asiyemuamini Allaah na Siku ya Mwisho" na at-Taawoos akasema kama hivyo na 'Ataa akasema: "Ni ukafiri usiokuwa ukafiri, dhulma isiyokuwa dhulma, na ufasiki usokuwa ufasiki. Na miongoni mwao ni wale wenye kuifasiri Aya kumaanisha Mwenye kuzikataa hukmu za Allaah haliyakuwa anazipinga na kuzikataa (jahidan lahu) nah ii ni kauli ya Ikrimah! Na huu ni msemo wenye dosari, kwani kule kukataa kwenyewe (juhud) ni ukafiri, pasi na kujali iwapo amehukumu kwayo au hakuhukumu. Na miongoni mwao ni wale waliofasiri kumaanisha kukataa kuhukumu kwa kila ambalo Allaah ameliteremshia hukmu yake, akasema na yoyote mwenye kuingiza kwenye mas'ala haya hukmu ya Tawheed na Uislamu!
Hii ni tafsiri ya Abdul-Aziz al-Kinani, na huyu nae yuko mbali na ukweli ulivyo!! Kwani utisho (ulio ndani ya Aya) ni kwa kukataa kuhukumu kwa sheriya iliyoteremshwa, na hii inaweza kumaanisha kuziachilia mbali sheriya kwa ujumla au baadhi yake tu.
Na baadhi yao ni wale wenye kuifasiri kwa maana ya kuhukumu kinyume cha maandiko yalivyo, tena kwaq kukusudia, pasi na kuwa ni mjinga nayo na wala sio kwa makosa katika kuyafahamu au kuyafasiri. Al-Baghawee ameyanukuu haya kutoka kwa wanavyuoni kwa ujumla.
Na miongoni mwao ni wale wenye kuyaeleza yakwamba yanawahusu Ahlul-Kitaab. Na huu ni msimamo wa Qataadah. Adh-Dhahhaak na wengineo. Na haya yako mbali (na ukweli ulivyo) – na ni kinyume cha matamshi yaliyo wazi kwahiyo hayafai kufuatwa kuwa ni ushahidi.
Na miongoni mwao ni wale wenye kuyaeleza kumaanisha ukafiri wenye kumtoa mtu nje ya Dini! **Na la sawa ni kwamba** kuhukumu kwa yasiyokuwa aliyoyateremsha Allaah ni sampuli mbili za Kufr (ukafiri) ; - kufr asghar (Ukafiri mdogo) na kufr akbar (ukafiri Mkubwa) – na (ama ni upi miongoni mwa sampuli hizo mbili) inategemea hali ya kiongozi. Ikiwa anaamini juu ya uwajibikaji wa kuhukumu kwa yale aliyoyateremsha Allaah katika hali hii lakini akawachana nayo hukmu hiyo – kwa ku'asi kwake – na haliyakuwa anakubali yakwamba anastahiki adhabu, basi huo ni ukafiri mdogo (kufr asghar). **Na iwapo yeye (l'taqada) anaamini yakwamba si wajibu na kwamba yeye ana khiyari kwenye suala hilo** – pamoja na imani yake thabiti yakwamba ni hukmu ya Allaah – basi huu ni ukafiri Mkubwa (kufr Akbar) na iwapo alikuwa ni mjinga kwenye mas'ala hayo au alifanya makosa, basi yeye atakuwa ni mwenye kukosea (mukhtee') na hukmu yake itakuwa ni sawa na wale wenye kukosea (yaani; atapata malipo mara moja).
Na malengo hapa ni kwamba madhambi yote ni aina ya ukafiri mdogo (kufr asghar). Kwani hayo ni kinyume cha shukrani – ambayo ni kufanya amali kwa kumridhisha Allaah. Na kujitahidi (kwa mtu), emma kutaleta shukrani (shukr) au ukafiri (kufr), au jambo la tatu ambalo si hili wala si lile (shukrani wala ukafiri) na Allaah yanamuelea Zaidi.

Mlango:
Ama kuhusu Ukafiri mkubwa (kufr akbar) – basi ni sampuli tatu: Kufr ya Takdheeb (kukataa); kufr kutokana na ujeuri na kiburi haliyakuwa mtu anaijua haki (tasdeeq); kufr ya I'raad (kupa mgongo); kufr ya shakk (kuwa na

YALIYOMO

HUKMU ZA ALLAAH 1 - 2

MAMA ZAO WAUMINI 2 - 4

shaka); na kufr ya nifaaq (unafiki). Kwahiyo kufr ya takdheeb – ni kuamini katika kuwakadhibisha Mitume, na sampuli hii ni chache sana kwa makafiri kwani Allaah aliwasaidia Mitume wake na akawapa dalili zenye kuwatilia nguvu ukweli waliokuja nao ambao ushahidi wa kisawasawa, na ambao wenye kuumaliza nyudhuru zote. Allaah akasema kumuhusu Fir'auni na watu wake: **"Na wakazikanusha, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo (ukweli wake)."** [27:14].

Kufr ya istikbaar na ibaa' (jeuri na kiburi) – basi hiyo ni kama kufr ya Iblees kwani hakukaidi/hakukataa amri ya Allaah na wala hakupingana nayo. Lakini alijitokeza kupambana nayo kwa ujeuri na kiburi – na kutokana na hayo ukaja ukafiri wa mwenye kutambua ukweli wa Mtume na kwamba amekuja na haki kutoka kwa Allaah, lakini hakuyakubali kutokana na kiburi na jeuri. Na kwa kawaida jambo hili ni ukafiri wa maadui wa Mitume, kama alivyosema Allaah kumnukuu Fir'aun na watu wake: **"O! Tuwaamini watu walio mfano wetu na ambao jamaa zao ni watumwa wetu?"** [23:47] na maneno ya mataifa mbalimbali kwa Mitume wao: **"Hamkuwa nyinyi ila ni watu kama sisi."** [14:10] na maneno yake: **"Kina Thamudi walikadhibisha kwa sababu ya upotofu (upotevu) wao."** [91:11], huu ni ukafiri wa Mayahudi, kama alivyosema Allaah: **"Na kilipowafikia kitabu kitokacho kwa Allaah kisadikishacho yaliyo pamoja nao (walikadhibisha)."** [2:89]. Na akasema: **"wanayafahamu haya kama wanavyowafahamu watoto wao."** [6:20]. Na huu pia ni kama ukafiri wa Abu Twaalib aliyemuamini (mtume) na wala hakuwa na shaka kuhusu ukweli wake lakini ukaidi ukamshinda nguvu pamoja na kujitwaza kwa babu zake, yakwamba asiwachane na dini yao na ashuhudie kwenye ukafiri wao.

Na ama kuhusiana na kufr ya I'raad (kupa mgongo) – basi huko ni kugeuka kando kwa masikio na moyo wake kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) – wakawa hawamuamini wala hawamkatai – wasijiunge nae na wala wasimfanyie uadui – na wala wasiyajali mambo aliyokuja nayo kama mmojawapo miongoni mwa Banu Abd Yaaleel alivyomwambia Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Wallaahi, mimi nitakwambia neno ambalo: Iwapo wewe ni mkweli, basi utakuwa ni mkubwa mno mbele ya macho yangu mpaka ibidi nikujibu, na iwapo unasema urongo, basi wewe utastahiki kudharauliwa mpaka ibidi (hata) mimi nisizungumze na wewe.

Na ama kuhusu kufr ya Shaqq (kuwa na shaka) – basi hapo ni pale mtu asipokuwa na uhakika na (kwa Mtume) ukweli na wala hamuamini – lakini akawa na shaka. Na shaka yake hii haitoendelea mpaka akusudie kuzipa mgongo alama za Allaah (ayaat) zenye kuhusiana na ukweli wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa ujumla, kiasi cha kwamba akawa hawasikii na wala hawageukii na kuwasikiza. Lakini iwapo angeliwageukia na kuwasikiza basi hapangekuwa na shaka yoyote kwake, kwani hizo (alama - ayaat) zingeshurutisha kupatikane ukweli, hususan ukweli wote kwa ujumla. Hii ni kwa sababu ishara zao za ukweli ni kama ishara za kuwepo kwa Jua yakwamba ni mchana.

Na ama kuhusu kufr ya Nifaaq (unafiki) – basi hapo ni pale anapodhihirisha Imani kwenye ulimi wake na kuficha ukanushaji ndani ya moyo wake na huu ni unafiki mkubwa zaidi.

MAMA ZAO WAUMINI

[Sehemu ya PILI]

Na: Dr. Muhammad Al-Jibaaly

Endelea kutoka Vol.17, Issue 5

VITA VYA AL-JAMAL (NGAMIA)

Katika tarehe 18 wa mwezi wa Dhul-Hijjah, mwaka wa 35 H, 'Uthmaan (رضي الله عنه) aliuwawa kutokana na hila za 'Abdullah Bin Saba' na maadui wengine wa Uislamu.

Siku chache baadae, Ali (رضي الله عنه) alichaguliwa kuwa Khalifa mpya. Ali, 'Aaisha na baadhi ya Maswahaba wengine wakubwa, wakakusudia kusuluhisha matatizo kufuatia mauwaji ya 'Uthman (رضي الله عنه) - muhimu zaidi, kuwatafuta wauwaji na kuustawisha (kuurudisha) tena ukhalifa. Kwa hali yoyote ile, Ibn Saba' na wafuasi wake waliendelea na njama zao, hatimae wakafaulu kuwafitini maswahaba na kuanza kupigana wenyewe kwa wenyewe, akiwemo 'Aaisha, Talhah na az-Zubayr (رضي الله عنهم) upande mmoja huku dhidi ya 'Ali,'Ammar na Maswahaba wengine (رضي الله عنهم). Vita hivyo vikaitwa vita vya al-Jamal (vita vya ngamia), kwa sababu vilipiganwa kwenye sehemu ya ngamia alobeba kiti cha 'Aaisha (رضي الله عنها).

Vilitokea vita hivyo katikati ya mwezi wa Jumaada al-akhirah, mwaka wa 36H. Ali (رضي الله عنه) akashinda vita hivyo, lakini baada ya takriban zaidi ya Waislamu 10,000 (elfu kumi) wakiwemo Talhah na az-Zubayr waliuwawa. Baada ya kushinda vita hivyo, Ali alimhudumia 'Aaisha kwa heshima na akamshindikiza kwa usalama hadi nyumbani kwake. 'Ammar Bin Yaasir (رضي الله عنه) alisema kwenye khutba aloitoa kabla ya vita hivyo, "Kwa kweli, sisi tunatambua yakwamba, yeye 'Aaisha ni mkewe Mtume wetu (صلى الله عليه وسلم) kwenye maisha ya mwanzo na mwisho."

Kuhusika kwa 'Aaisha na wafuasi wake kwenye vita hivyo kumetokamana na ijitihad, na walifanya hayo kwa kumridhisha Allaah. Lakini, waligundua baadae yakwamba msimamo wao huo ulikuwa ni wa makosa, na akajuta 'Aaisha majuto makubwa mpaka siku zake za mwisho.

MAUTI YA 'AAISHA (رضي الله عنها)

'Aaisha (رضي الله عنها) aliiwasilisha sehemu kubwa sana ya elimu kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na idadi ya Maswahaba zake, wakiwemo Abu Bakr na Umar (رضي الله عنهم). Masimulizi yake yaliyohifadhiwa ni zaidi ya elfu mbili na mia tatu ambayo yamehifadhiwa katika al-Bukhari, Muslim au wote wawili. 'Aaisha (رضي الله عنها) alikuwa ni mwanamke mtoaji, na mkarimu na aliishi maisha ya wastani.

'Aaisha (رضي الله عنها) alikufa katika mwaka wa 57H huko al-Madina na akazikwa al-Baaqi'.

ZAYNAB BINT KHUZAYMAH

Bibi Zaynab Bint Khuzaymah Bin Al-Harith Bin 'Abdillah Al-Hilaaliyyah (رضي الله عنها) pia akiitwa kwa jina la Ummul-Masaakin (mama wa maskini) kutokamana na ukarimu wake wa kutoa kwa wingi. Yeye ni nduguye Maimunah kwa upande wa mama. Awali, aliolewa na at-Tufayl Bin Al-Harith. Baada ya kufa at-Tufayl, aliolewa na nduguye 'Ubaydah Bin Al-Harith. Nae 'Ubaydah aliuwawa kwenye vita vya Uhud, na Mtume (صلى الله عليه وسلم), mapema baada ya tukio hilo, akamuowa.

Aliishi na Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwa takriban muda wa miezi miwili pekee kisha akafariki alipofika umri wa miaka thalathini. Alikuwa ni wa mwanzo miongoni mwa mama za Waumini kuzikwa katika makaburi ya al-Baqi'.

UMM-SALAMAH

Nasaba yake: Jina la Umm Salamah (

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Continued from page 2)

رضي الله عنها) lilikuwa Hind Bint Abi 'Umayyah. alitokamana na kizazi cha Makhzum cha kabila la Quraysh. Alikuwa ni binamu wa Khalid Bin Al-Walid na
Abu Jahl Bin Hisham. Alikuwa ni mwanamke mzuri sana atokae kwenye nasaba ya kuheshimika mno. Alikuwa ni miongoni mwa Waislamu wa mwanzo wa kike waliohama kuelekea al-Madina kabla ya kuolewa na Mtume (صلى الله عليه وسلم), aliolewa na nduguye wa kunyonya, (kulea), Abu Salamah Bin Abd il-Asad Al-Makhzum (رضي الله عنه)

KUOLEWA KWAKE NA MTUME (صلى الله عليه وسلم)

Umm Salamah akahadithia yakwamba siku moja alimsikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema:**'Pindi msiba unapompata Muislamu na akasema kama alivyoamrishwa na Allaah, "Hakika sisi ni wa Allaah, na kwake Yeye tutaregea, Ewe Allaah, nijazi kwa yaliyonisibu na unipe badala yake kwa yaliyo bora." Basi kwa hakika Allaah atampa badala yake kwa yaliyo bora.'**
Hivyo basi, alipokufa Abu Salamah, Umm Salamah akaanza kufikiri, "Ni yupi miongoni mwa Waislamu atakuwa bora kuliko Abu Salamah? Yeye alikuwa ni katika wa mwanzo kuhamia kwa ajili ya Mtume (صلى الله عليه وسلم)! Mbali na yote hayo aliomba du'a
Hiyo na Allaah akamtakabaliya kwa kumpa Mtume (صلى الله عليه وسلم) badala ya Abu Salamah. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimpa ujumbe Haatib Bin Abi Balta'ah ende akamposee bibi huyu (Umm Salamah) nae akajibu, "Mimi ninae binti yangu (namlea) nami ni mwanamke mwenye wivu (na wewe umeowa wake wengi)." Kwa hivyo Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: **"Amma kuhusu binti yake, tunamuomba Allaah amtoshelezee kutokamana na yeye (mama). Na namuomba Allaah amuondoshee wivu alonao."**
Kwenye riwaya nyengine, Umm Salamah (رضي الله عنها) ametueleze yakwamba alipokufa Abu Salamah alikwenda kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akamwambia, "Ewe Mjumbe wa Allaah! Abu Salamah amekwisha kufa." Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia aseme: **"Ewe Allaah nisamehe mimi na yeye na umtangulize yeye badala yangu kwa lilo zuri."** Na akamalizia, "Allaah kisha akanipa mimi badala yake kwa alo bora kwangu kuliko yeye: Muhammad (صلى الله عليه وسلم)!".
Aliolewa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika mwaka wa 4H na hapo alikuwa na umri wa takriban miaka thalathini. Wanawe wote watatu, Umar, Salamah na Zaynab walikuwa Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Na yeye mwenyewe pia alikuwa ni miongoni mwa wanazuoni wa kiswahaba.

KIFO CHAE

Umm Salamah alikuwa ni wa mwisho wa mama za waumini kuaga dunia. Aliishi mpaka kufikia wakati wa kuuwawa kwa al-Husayn Bin Ali (رضي الله عنه). Jambo hilo lilimuhuzinisha sana nae akaaga duniya muda mfupi baada ya tukio hilo. Na hapo ilikuwa ni mwaka wa 61H akiwa na umri wa tisiini kwa makisio. Alizikwa kwenye makaburi ya Al-Baqi`.

HAFSAH BINT 'UMAR

Hafsah (رضي الله عنها) alikuwa ni binti yake 'Umar Bin Al-Khattaab Bin Nufayl (رضي الله عنه) kutoka kwenye kizazi cha Quraysh. Mamake alikuwa ni Zaynab Bint Maz'un ambae ni dadake 'Uthmaan Bin Maz'un. Hafsah aliwahi kuolewa mbeleni na Khumays Bin Hudhaafah as-Sahmi. Huyu Khumays alikuwa ni miongoni mwa Waislamu wa mwanzo waliohajiri kwenda al-Habashah (Abyssinia). Alijumuika kwenye vita vya Badr na Uhud, na akafa kutokana na majaraha mapema baada ya vita vya Uhud katika mwaka wa tatu wa al-Hijrah. Baada ya kifo cha Khumays, 'Umar, akataka kumuoza Hafsah kwa Abu Bakr na 'Uthmaan, lakini wote wakakataa kumuowa. Jambo hilo likamuudhi 'Umar, lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamtuliza kwa kumwambia: **"Mtu alie bora kuliko 'Uthmaan atamuowa Hafsah, na 'Uthmaan atamuowa alie bora kuliko Hafsah."** Hafsah alipo-olewa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa na takriban umri wa miaka ishirini. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimtaliki(alimwacha) talaka moja, yamkini kwa kufichua siri aloamrishwa kuhifadhi na Mtume (صلى الله عليه وسلم) (kama
Tutakavyoizungumzia hapo chini), lakini Allaah akamuamrisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) amrudie. Akasema, **"Jibril ameniambia, "Mrudie Hafsah, kwa sababu anafunga sana na kuswali swala za usiku, nae atakuwa ni mkeo kwenye Jannah (Pepo)."**
Aliaga duniya takriban mwaka wa 41H akiwa Al-Madina.

ZAYNAB BINT JAHSH

Zaynab Bint Jahsh Bin Rayaab (رضي الله عنها) alikuwa ni binti ya Umaymah bint 'Abd ul-Muttalib Bin Hashim, shangazile Mtume (صلى الله عليه وسلم) upande wa baba. Alizaliwa takriban miaka 20 kabla ya kuanza shughuli za Utume. Alisilimu akiwa Makkah mapema wakati wa harakati za Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akaozwa Zayd Bin Haarithah, Mawlaa (huria) wa Mtume wa Allaah. Ndoa yao haikufana na ilimalizikia na talaka. Baada ya kuachwa, bila ya kukawiya, ikaja amri
kutoka kwa Allaah yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amuowe. Alikuwa akijivunia kwa hilo na akisema: "Nyinyi muliozwa na wazazi wenu; amma kunihusu mimi, Allaah Ndie alienioza kutoka juu ya kiti Chake."
Alikuwa ni mke mwema,mwenye huruma na mtoaji. Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم) : **"Wakwanza miongoni mwenu (wake zangu) atakaejiunga na mimi ni yule mwenye mikono mrefu (mtoaji sana)."** 'Aaisha (رضي الله عنها) akasema: "Wote wao (Mama za waumini) walikuwa wakishindana katika utoaji, lakini Zaynab alitushinda kwa sababu alikuwa akifanya kazi (akipata pesa) na kisha akizitoa kwa njia ya sadaka." Kwa hivyo, imeelekea yakuwa hadithi hiyo imemhusu yeye, kinyume na baadhi ya waandishi wanavyodhania (kuwa imemuhusu Sawdah).
'Aaisha (رضي الله عنها) vile vile akamsifu kwa kusema: "Alikuwa ni mshindani wangu mkubwa katika kujipendekeza kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Sijaonapo mwanamke mwema zaidi ya Zaynab, wala mwenye taqwa ya Allaah, alo mkweli alo-mkarimu mbele ya jamaa zake, mwenye fadhila, na alo na bidii juu ya kazi aloifanya kwa njia ya sadaqa... isipokuwa kwa hasira alizokuwa nazo, lakini akijizuia kwa haraka.
Allaah amuelee radhi." Hadith hiyo hapo juu yaonyesha yakuwa Zaynab alikufa kabla ya Sawdah. Alikufa mwaka wa 20H na 'Umar (رضي الله عنه) akamswalia. Alizikwa al-Baqi`.

JUWAYRIYAH BINT AL-HAARITH

Juwayriyah (رضي الله عنها) alikuwa ni binti ya al-Haarith Bin Abi Diraar. Alikuwa akiitwa Barrah, lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) akalibadilisha jina hilo na kumwita Juwayriyah. Kabila lake ni Al-Mustaliq, na alichukuliwa kama mfungwa wa kivita wakati wa vita vya Al-Muraysi' mnamo mwaka 5H. Alipo-olewa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa na Umri wa miaka ishirini na akafa baada ya takriban miaka 50.
Alikuwa ni mwanamke mrembo sana

(Continued on page 4)

(Continued from page 3)

kama alivyoungama mkewe mwenza 'Aaisha (رضي الله عنها): "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipowagawanya wafungwa wa kivita wa kabila la al-Mustaliq, Juwayriyah Bint al-Haarith alipewa Thaabit Bin Qays Bin Ash-Shammaas
(au Binamu yake). Juwayriyah akafanya mkataba nae ili ajikomboe kwa pesa. Alikuwa ni mwanamke mrembo sana, hapana yeyote atakaemuona isipokuwa ataduwaa kwa urembo wake. Alikuja kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kutaka msaada wake ili ajikomboe. Wallahi, nilipomuona amesimama mlangoni kwangu, nilimchukia (kwa urembo wake), na nikajua tu yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) ataona kitu kwake yeye
nilichokiona mimi (cha urembo). Aliingia ndani akasema,"Ewe Mjumbe wa Allaah! Mimi ni Juwayriyah Bint al-Haarith Bin Abi Diraar, kiongozi wa watu wake, na nimeguswa na mkasa kama ujuavyo. Nimegawiwa kwa Thaabit Bin Qays Bin Ash-Shammaas (au Binamu yake). Nimefanya mkataba nae ili nijikomboe, na nimekuja kutaka msaada wako kuhusu jambo hilo. Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم), **"Jee, ungelipendelea kupata lilo bora kuliko hilo?"** 'akauliza 'Ni kitu gani hicho, Ewe
Mjumbe wa Allaah?' Akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم), **"Nitakulipia deni hilo, kisha nikuowe."** Akasema Juwayriyah "Bila shaka! Ewe Mjumbe wa Allaah." Akasema (صلى الله عليه وسلم), **"Hilo limeshapita".** Habari ziliposambaa yakwamba Mjumbe wa Allaah amemuowa Juwayriyah, Waislamu wakawaacha huru wale wafungwa wa kabila la al-Mustaliq, ambao wameshakuwa ni shemegi zake. Hivyo basi, jamii mia moja kutoka kwenye kabila la al-Mustaliq ziliachwa huru, na sijawahi kuona mwanamke yeyote aliwahi kuwaletea baraka watu wake zaidi ya Juwayriyah alivyo fanya.

UMM HABIBAH

Jina lake Umm Habibah (رضي الله عنها) lilikuwa ni Ramlah Bint Abi Sufyaan. Jina la Abu Sufyaan lilikuwa ni Sakhr Bin Harb Bin Umayyah Bin Abd Shams Bin Abd Minaf Bin Qasiyy. Vilevile Umm Habibah alikuwa ni dadake Mu'awiyah Bin Abi Sufyaan. Alikuwa yeye (Umm Habibah) ni Binamu yake Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuumeni na alikuwa na uhusiano nae zaidi kuliko wake zake wote. Alihajiri kuelekea al-Habasha (Abyssinia) pamoja na muwewe 'Ubaydullah Bin Jahsh. Walipokuwa al-Habashah,
mumewe alirudi na akafa kafiri. Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamtumiliza 'Amr Bin Umayyah kwenda kwa an-Najaashi akamuoza Mtume (صلى الله عليه وسلم) akampa dirham elfu nne na kumtunukia zawadi na akampeleka al-Madina akiandamana na Sharhabil Bin Hasanah kama mlinzi wake. Aliwasili al -Madina katika mwaka wa sita wa Hijriya, akiwa na umri wa zaidi ya miaka thalathini. Alikufa chini ya utawala wa nduguye Mu'awiyah mnamo mwaka wa 42 au 44H.

SAFIYYAH BINT HUYAYY

Safiyyah Bint Huyyay Bin Akhtab Bin Sa'yah (رضي الله عنها) alitokamana na kizazi cha Mtume Harun (عليه السلام), ambae nae alitoka kwenye kizazi cha Laawi Bin Yaqub Bin Is-haaq (عليه السلام). Hapo awali, Bibi Safiyyah, aliolewa na Salaam Bin Abi al-Haqiq, na kisha akaolewa na ndugu yake Kinaanah Bin Abi al-Haqiq. Kinaanah akauwawa kwenye vita vya Khaybar na Safiyyah akashikwa kama mfungwa wa kivita, lakini Mtume
(صلى الله عليه وسلم) akamuachilia huru na akamuowa. Hapo alikuwa na takriban umri wa miaka kumi na saba.
Alikuwa ni mwanamke bora, mwenye heshima, busara na mke mwema anaependeza. Siku moja, Anas akatuahidithia yakwamba Safiyyah alimsikia Hafsa akimsema: "Yeya si chochote bali ni binti ya kiyahudi." Akaanza kulia kutokana na matamshi hayo na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamuuliza kuhusu kinachomliza. Alipomueleza vile alilyosema Hafsah, Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: **"Kwa hakika wewe ni binti ya Mtume (Harun); na kwa hakika mjombako (Musa) ni Mtume; na kwa hakika wewe mwenyewe umeolewa na Mtume. Kwa hivyo, ni kwa nini anajigamba juu yako?".** Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamwambia Hafsah, **"Mche Allaah, Ewe Hafsah."**
Alifariki dunia takriban kwenye mwaka wa 50H. akiwa al-Madina na akazikwa al- Baqi`.

MAYMUNAH BINT AL-HARITH

Maymunah Bint Al-Harith Bin Hazn Al-Hilaaliyyah (رضي الله عنها) alikuwa ni dadake Umm al-Fadhl, mkewe al-'Abbaas. Hivyo basi, alikuwa ni shangazi yake Khalid Bin al-Walid na Ibn Abbaas (رضي الله عنه).
Kabla ya Uislamu, Maymunah, aliolewa na Mas'ud Bin 'Amr ath-Thaqafi ambae
baadae alimuacha. Kisha akaolewa na Abu Ruhm Bin 'Abd il-'Uzza. Alipokufa Abu Ruhm, aliolewa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika mwaka wa 7H, Dhul-Qa'adah mapema baada ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kufanya Umrah. Alikuwa ni mwanamke mwenye tabia nzuri sana. 'Aaisha akamsifu kwa kusema: "Wallahi, Maymunah sasa ameshatuondokea. Kwa hakika, hapana shaka yakwamba alikuwa ni muadilifu zaidi miongoni mwetu na mwenye huruma kwa jamaa zake." Alifariki mwaka wa 50H na akazikwa Sarif, pambizoni mwa Makkah palepale mahali aliko olewa na Mtume (صلى الله عليه وسلم).

MARIYA AL-QIBTI

Mariya Bint Sham'un (رضي الله عنها) alikuwa ni miongoni mwa watumwa wa kike wa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Aliekuwa mfalme wa Alexandria na Misri, Al-Muqawqas, ndie aliemtunukia Mtume (صلى الله عليه وسلم) Bibi Mariya kama tunu kwenye mwaka wa 7H. Asli yake ni Mqibti kutoka Misri na ana rangi ya kutakata. Alisilimu alipofika al-Madina. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamvisha utaji na kumuhifadhi kama wakeze wengine, nae akamzalia kijana akamwita Ibrahim katika mwaka wa 8H. Jambo hili likamfidia kuwa huru. Ibrahim alifariki alipotimia umri wa miaka miwili.
Bibi Mariya alifariki mwaka wa 16H, wakati wa khilafa ya 'Umar (رضي الله عنه) na akazikwa al-Baqi`.

WAKE WENGINE

Kulikuwepo na wanawake wengine walio-olewa na Mtume (صلى الله عليه وسلم), lakini kutokana na sababu mbali mbali hakuwahi kuwaingilia.
Wanawake hao ni:

1. Al-'Aliyah kutoka katika kabila la Bakr Bin Kilaab.
2. Asmaa' Bint Ka'b al-Jawniyyah.
3. Umm Shariik kutoka kabila la al-Ansaar.
4. Sanaa' Bint Asmaa' Bin as-Salt-as-Sulamiyyah.
5. Fatimah al-Kilaabiyyah.
6. Asmaa' Bint an-Nu'maan al-Kindiyyah.

Amma kuhusu huyo mwanamke wa pili alietajwa hapo juu, 'Aaisha (رضي الله عنها) akatuhadithia yakwamba al-Jawniyyah alipoingia nyumbani kuonane na
Mtume (صلى الله عليه وسلم) na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamkurubia, alisema, ("Audhu Billahi Mink- Najilinda kwa Allaah na wewe"). Pale pale Mtume (صلى الله عليه وسلم) akampa talaka akasema: **"Kwa hakika umeomba ulinzi wa kutoka kwa Alie-tukuka: Nenda kwa jamaa zako".**
Riwaya nyengine ziliashiria yakwamba (Mwanamke huyo) alijuta kwa kitendo hicho maisha yake yote.